

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



TANGAZO

UTHIBITISHO WA MATOKEO (STATEMENT OF RESULTS) KWA WATAHINIWA WENYE VYETI VISIVYO NA PICHA

Baraza la Mitihani la Tanzania, linapenda kuwajulisha kuwa, limeanza kutoa Uthibitisho wa Matokeo (**Statement of Results**) kwa kuwakabidhi watahiniwa husika waliopoteza vyeti badala ya kutuma kwa waajiri kama ilivyokuwa hapo awali. Uthibitisho huo utakuwa ni waraka wa kudumu utakaowaondolea watahiniwa usumbufu wa kuomba upya kila inapohitajika. Huduma hii itawahusu watahiniwa wa Kidato cha **Nne** wa kabla ya mwaka **2008** na wa Kidato cha **Sita** na **Ualimu** wa kabla ya mwaka **2009** ambao hawana sifa za kupata vyeti mbadala.

Fomu ya maombi ya Uthibitisho wa Matokeo inapatikana katika ofisi za Baraza zilizopo Dar es Salaam na Dodoma ama kwa kupitia tovuti ya Baraza www.necta.go.tz. Aidha, vielelezo vinavyotakiwa pamoja na gharama ya huduma vimeorodheshwa kwenye fomu husika. Mtahiniwa anashauriwa kujaza fomu kikamilifu na kuiwasilisha katika ofisi za Baraza au kwa kuituma kwa **Katibu Mtendaji**, Baraza la Mitihani la Tanzania, S.L.P 2624, Dar es Salaam au itumwe kwa barua pepe esnecta@necta.go.tz.

Limetolewa na:

KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA